# *USHIRIKA*

Asante, Ndugu Joseph.

2 Mwaweza kuketi. Habari za jioni, marafiki. Nina furaha sana kuwa hapa Chicago alasiri ya leo ku—kuzungumza na kundi hili zuri la watoto wa Mungu. Na inaonekana nzuri sana kusimama nyuma ya mimbara tena. Hii imekuwa siku kadhaa. Nilikuwa nimeketi chumbani mle, nikingoja dakika chache zilizopita; basi mlipoanza kuimba *Amini Tu* Billy akageuka akanitazama. Mimi. . .Chozi dogo lilidondoka ndani ya moyo wangu. Sijui kama mnajua ninachomaanisha au la, kwa ndani: kusikia wimbo huo tena, *Amini Tu*. Nami nikawazia, "Hiyo ni mara nyingine tena ninaenda jukwaani."

3 Tuliendesha gari huku asubuhi ya leo, tukaingia muda mfupi tu uliopita, kisha tukafika hapa. Na kwa hiyo, mimi. . .sababu ya mimi kuwa hapa leo, moja ya hizo sababu, ni bila shaka, kuwaona ninyi wapendwa. Sikuzote napenda kuja Chicago. Ninajisikia niko nyumbani kabisa sasa. Hiyo ni. . .Sina haja ya kusema hivyo a—alasiri hii, lakini huo ndio ukweli. Na kisha kupata kukaa, kuwa pamoja na Ndugu yangu Boze.

Nami nilimsikia. Alinipigia simu, hivi majuzi, na kusema, "Je, unaweza kuja Jumapili?"

4 Nami nikasema, "La, siwezi kufanya hivyo, Ndugu Joseph." Nikasema, "Ninaninii tu, mke wangu anatarajia m—mtoto mchanga wakati wowote." Nikasema, "Kamwe nisingeweza kwenda."

Akasema, "Naam, nilikuwa niondoke. Ninaenda kwenye nchi za ng'ambo," kisha kasema, "Mimi. . . "

5 Nikasema, "Nitakuja kusema 'kwaheri,' au, 'hata tuonane,' ndivyo tusemavyo, kwa mtindo wa wahubiri. Hatuambiani kwaheri, kwa sababu tutaishi pamoja milele. Kwa hiyo sisi—sisi husema tu "hata tuonane" mpaka aende kule, na kumtakia baraka za Mungu, na kupata kusema hivyo mbele ya kanisa hapa.

6 Ndipo basi, nilifikiri, labda, kwamba kama nilivyopata kusema mbele yake na kanisa, kwa kawaida, katika ibada hizi za uponyaji nilizo nazo, sipati nafasi ya kujieleza, hisia zangu, kwa watu jinsi ninavyotaka, nilitaka kulielezea kanisa hili, alasiri ya leo, kwa njia bora zaidi niliyo nayo, ambayo ni duni sana, lakini, shukrani zangu kwa Ndugu Boze, mchungaji wenu.

Mimi. . .Nikililelezea kama ninavyomwelezea mke wangu. Nilisema, "Kuna maskini Mswidi mmoja ninayempenda kweli."

7 Yeye hu—huniita "Tugu Branham," nami namwita "Yosefu." Kwa hiyo m—mnajua sisi ni marafiki wa aina gani. Na

huyu tutakayempata ni mvulana. Jina lake litakuwa Joseph, pia. Hiyo—hiyo ni kweli. Kwa hiyo kweli tu—tunamthamini Ndugu Joseph; yeye. . . Si kwa sababu ameketi hapa, hiyo ni. . . Kama angekuwa ameondoka ingekuwa bora zaidi. Lakini nina marafiki wengi wazuri na waaminifu ambao hakika ninawaheshimu sana.

8 Nikija tu muda mfupi uliopita, nikija kwenye Barabara ya Pwani ya Kusini, nadhani mnaita hivyo huko, kile. . . Mimi na Billy tulikuwa tunazungumza, naye akasema, "Unarudi usiku wa leo, Baba?"

Nikasema, "Nitakuwa nimechoka mno, Billy." Nikasema, "Nitahubiri mara mbili, nadhani, leo," kisha nikasema, "Itakuwa. . . Nitakuwa nimechoka sana."

9 Akasema, "Wajua nini?" Kasema, "Nafikiri Ndugu Boze ni mmoja wa—mmoja wa watu wazuri sana ambao nimewahi kukutana nao." Nitalisema kwa maneno ya mvulana wangu, "Vivyo hivyo." Hiyo ni kweli.

10 Nimetokea kumpenda Ndugu Joseph. Haya ndiyo ninayopenda juu yake, mambo mengi: kwanza, kwa kuwa ni ndugu Mkristo; pili, unaweza kutegemea anachosema. Napenda hilo. Ninapenda mtu ambaye anapokuambia jambo lolote, atasimama nalo. Jambo lingine ni hili: yeye ni rafiki yangu niwe sahihi au nisiwe sahihi. Sasa, mtu yeyote anaweza kuwa rafiki yako wakati uko sahihi. Lakini wakati ukiwa makosani, basi yeye bado ni rafiki yako. Sasa, siko sahihi nyakati zote. Mnajua? Sehemu kubwa ya wakati mimi, labda, nimekosea. Lakini kama nimekosea au niko sawa, Joseph Boze ni rafiki yangu. Nimemwona katika majaribu makali. Nimemwona katika nyakati ambazo umma haujui chochote juu yake, tunapokabiliana na wakati wa majaribu. Daima amesimama karibu nami kama ndugu nami ninathamini hilo sana.

Nimeninii. . . Hakika kumekuwako na watu waliojaribu kunivunja moyo, waliosema, "Ndugu Joseph ni wa Watakatifu wa Siku za Usoni," au, "Wa Siku za Usoni. . . " Wanaitwaje? Mvua ya Siku za Usoni?

Nikasema, "Sijali kama yeye ni wa kwanza, wa pili, wa usoni, au wa katikati kabisa. Yeye—yeye ni ndugu yangu."

11 Kuja kwetu pamoja. . . Wakati mmoja mkutano ulikuwa karibu kufutiliwa mbali huko Chicago, Illinois, katika mkutano wa hema, kwa sababu wao. . . Sijawahi hata kumwona maishani mwangu, nilifutilia mbali mkutano wa hema kwa sababu wasingeuunga mkono mkutano wa Ndugu Joseph. Ninyi nyote hamjui hilo, bali hiyo ni kweli.

Nilikuwa tu nimerudi kutoka Stockholm, Uswidi, ndipo kundi ambalo lilikuwa pamoja nami, likasema. . . Nikasema, "Je, huu ni ushirikiano kamili wa makanisa yote?"

“Naam.”

12 Nami nikasema, “Maskini jamaa yule wanayemnena huko juu. . . ” Ni lipi lile ka—kanisa la Kiswidi kule, alilolijua Ndugu Pethrus? Nikasema, “Je, anashirikishwa?”

13 Vema, yule jamaa aliyekuwa akizungumza nami, akasema, “La. Unaona, Ndugu Branham, inge—ingeidhuru mikutano yako,” kasema, “kwa sababu yeye ni wa Mvua ya Siku za Usoni.”

14 Nikasema, “Ikiwa hawezi kuwa huko, na mimi pia siwezi.” Hamna lingine. Nikasema, “Kama sisi hatuyabagui madhehebu, hiyo inamaanisha ni kila mtu; sijali ni nani. Kama ni Mmethodisti, Mbaptisti, Shahidi wa Yehova, yeyote yule, watakuwa kule kwa vyovyote vile. Wala hatuwezi kuchora mstari, na kusema mtu *huyu* hana haki, kwa sababu sisi ni ndugu kikamilifu pamoja, na hivyo ndivyo tunavyotaka kubaki.” Kwa hiyo haidhuru wanahudhuria kanisa gani, wao ni. . . sisi sote ni ndugu katika Kristo, na hapo ndipo tunapozaliwa mara ya pili kwa Roho. Nami ninamthamini Ndugu Joseph kwa moyo wangu wote.

15 Na halafu basi ninawazia tu. . . Sasa, sikuambiwa hili, wa—wala sina lolote nililowazia hapo kabla. Lakini ninawazia tu alipokuwa akizungumza nami pale, kwamba kabla hajaondoka, nikijua ya kwamba yeye ni maskini (anaishi tu kwa misaada ya watu kama nifanyavyo mimi), kwamba kabla hajaondoka labda wangechukua sadaka ya upendo kwa mtu huyo kabla hajaenda kule. Nilitamani ningeweza kufanya hivyo. Nilimwuliza muda mfupi uliopita. Nikasema, “Ndugu Joseph, utajichukulia sadaka ya upendo?”

Akasema, “Huenda ikawa, Ndugu Branham, usiku wa leo, pengine watafanya. . . ”

16 Nikasema, “Laiti ningekuchukulia, ndugu,” lakini nikasema, “ungefilisika kama ningekuchukulia.” Lakini nikasema, “Ni—ningependa tu. . . ” Hujawahi kunisikia nikisema. . . kutaja mambo hayo katika. . . kutoka jukwaani, kwa maana sijapata kuchukua sadaka maishani mwangu.

17 Lakini, ndugu, lolote ambalo ningeweza kufanya kumsaidia mtu huyo safarini, ningelifanya, kwa sababu, nitawaambia ni kwa nini. Nilipokuwa mahali pagumu, nyote hamjui lolote kulihusu; ulifanya hivyo. Nilikuwa hapa wakati mmoja, nikienda kwenye nchi za ng’ambo, na nikifanya matayarisho, nikiwa tayari kwenda, nimepungukiwa na dola elfu mbili ili kuwa na za kutosha kulipia tiketi (Hiyo ni kweli.), za kutosha kulipia tiketi. Lakini kwa imani, Mungu alikuwa ameniita na nilikuwa naenda. Naye Joseph, kwa uvuvio, sikumwambia kamwe, bali kwa uvuvio, alitoka nje na—na kuwashirikisha watu jambo hilo. Sio kulazimisha, kusema tu tulikuwa tukienda katika nchi za ng’ambo, na tunahitaji pesa za kuendelea, ama kitu kama hicho, naye akuchukua sadaka hiyo kutoka

Chicago. Kwa imani tuliichukua. Nikanunua tiketi kesho yake nikaondoka.

18 Nilitaka kusema, kwamba akienda kule, kila kitu tunachofanya usiku wa leo, Bwana mwema na ambariki sana na amtume. Sasa, labda hajawahi kuwa katika sehemu hii ya nchi hapo awali, sivyo, Ndugu Joseph, kule unakoenda? [Ndugu Boze anajibu, "Hapana."—Mh.] Yeye pia hatambui kabisa kile anachokabili. Kwa hivyo najua ni jambo gumu unapoingia Afrika. Naomba kwamba Mungu atakuwa pamoja na ndugu yangu na ambariki katika kila jambo; na naomba awalete watu kwa Kristo huko. Nami ninatumaini kwamba Bwana mwema atamwezesha kuwa na mkutano wenye mafanikio zaidi aliyowahi kuwa nayo maishani mwake mwote, na arudi Chicago, hivi karibuni, mwenye nguvu mpya, na kadhalika, na tayari kuwaletea ninyi habari za uamsho mkuu. Hii itamfanya kuwa mmishenari, atakapoenda wakati huu. Ninajua hilo kidogo linasikika la kigeni kwenu ninyi watu katika makanisa mengine.

19 Sikilizeni. Ninyi. . . Mmishenari si mtu anayebadili taifa lake la kuishi. Mmishenari ni mtu anayeenda na kurudi. Paulo alikuwa ndiye mmishenari mashuhuri kuliko wote ulimwengu uliyepata kujua. Hiyo ni kweli? Ukimfundisha tu mtu, na kumpeleka kule, na kufanya makazi yake kule, akae maisha yake yote, alibadili tu taifa lake. Huyo si mmishenari. Mmishenari anatoka sehemu moja hadi nyingine, na kwenda sehemu nyingine, na kuninii tu. . . Paulo alizunguka pande zote, kisha akarudi, na kutoka tena; sehemu zote na kurudi. Kwa hiyo Paulo alikuwa mmishenari. Ndugu Joseph, Mungu akurudishe salama kama mmishenari basi. Atakurudisha tena. Bwana akubariki.

20 Na kwenu ninyi watu wapendwa hapa Chicago, nilitaka kuuliza labda, je, kuna mgonjwa yeyote miongoni mwetu leo? Kama yupo, inua mkono wako, mtu fulani, ili labda mwe na mkutano wa maombi usiku wa leo, kuomba—kuwaombea wagonjwa. Ikiwa mnataka maombi kwa ajili ya wagonjwa usiku wa leo? Inueni mikono yenu, kila mtu, anayetaka mkutano, omba. . . Naam, sawa. Hilo ni zuri. Basi tutawaombea wagonjwa usiku wa leo. Nitawaachia kadi hapa watakazosambaza saa kumi na mbili na nusu, ama kitu kama hicho, nawe unaweza kushuka na kuchukua kadi yako ya maombi, nasi tutawaombea. . . [Ndugu Boze anasema, "Thenashara."—Mh.] Thenashara? Thenashara? ["Nao mkutano saa moja."] Naam. Vema, thenashara, basi, usiku wa leo, hiyo itakuwa sawa.

Sawa. Sasa. . . Jambo la kwanza, kama Billy Paul ananisikia, tafuta ndani ya gari uone kama tuna kadi zozote za maombi.

21 Hatuna, je, una zingine? Una kitu unachoweza kutengenezea zingine endapo hawana? Vema, sawa, hiyo itakuwa sawa. Vema,

basi usiku wa leo tu—tutawaombea wagonjwa.

22 Sasa, alasiri ya leo, tunachelewa, wala hatujaanza kamwe. Mnajua jinsi tulivyo, kidogo ni waenda pole kuanza, na kisha waenda pole kumalizia. Hiyo ni ninii. . . Lakini na—napenda tu kuja hapa na kuzungumza nanyi wapendwa. Nanyi mwe mkimwombea mke wangu mpendwa, je, mtafanya hivyo, kwa ajili ya maskini mtoto huyo anayekuja? Maskini mwanamke huyo, bila shaka ana wakati mgumu, nasi tunamtazamia Yeye Yule asiyeonekana kwa ajili ya ukombozi.

23 Sasa katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, ningependa kusoma maneno machache tu na kuzungumza nanyi kwa muda mfupi na—na. . . [Ndugu Boze anasema, "Saa iko kwenye. . . mkono wako wa kulia."—Mh.] (Loo, naam. Mbona, asante, ndugu.) Na sasa, tutajaribu kuondoka katika yapata dakika thelathini, Bwana akipenda, nataka kuzungumza nanyi leo. Hebu tusome kutoka kwenye Maandiko katika Yohana Mtakatifu, ama, si Yohana Mtakatifu, Yohana wa Kwanza, mlango wa kwanza.

24 Sasa, naona wako hapa chini, marafiki zangu, Leo na Gene, wavulana kadhaa kutoka katika ujirani wenu hapa, hurekodi. Na, aisee, jambo lingine, wavulana hawa huhudhuria mikutano yote na kurekodi, nao wanazo kwenye kanda. Niliagiza niletewe kanda. . . Mtu fulani alikuwa amehubiri mahubiri hivi majuzi, nami nikaagiza niletewe kanda. Jamani, nilifikiri itanilazimu kununua nchi nzima nipate hiyo kanda: yapata dola tisa kwa kanda. Nikawazia, "Loo, jamani." Niliwauliza hawa wavulana. Nikasema, "Vipi kuhusu hili?" Vema, jamani, kulikuwa na tofauti jinsi gani katika zile walizo nazo. Nao wana kila ujumbe, na kadhalika.

25 Ni za kijua kali, na za mlo wa ugali; bali zitakufaa; zitakusaidia sana. Imenileta salama umbali huu, niko tayari kuichukua. Nimeitumainia, katika uvuli wenyewe wa mauti, dini hii ya kale, iliniokoa. Huenda haijang'arishwa ipaswavyo, lakini nataka baraka za Mungu ziwe pamoja nami, haidhuru imeng'arishwa kiasi gani.

Na sasa. . . Naye Bwana na awabariki wavulana hawa wawili, ambao ndio kwanza wayatoe maisha yao kwa kusudi hilo, na kazi ya—yao.

26 Sasa, tunapaswa kuanzia kusoma kifungu cha 5, tushuke chini tukijumuisha kifungu cha 7.

> *Na, hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuhubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lolote hamna ndani yake.*
>
> *Tukisema ya kwamba tuna ushirika naye, na kuenenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli:*

*Lakini tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo Mwana wake* yatusafisha *dhambi yote.*

Hilo si linapendeza?

Sasa, twaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo?

27 Baba yetu wa Mbinguni, tukizungumza leo hii na kusanyiko hili zuri la watu wanaoelekea Umilele, labda wengi wao tayari wameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, wakayafanya mavazi yao meupe, safi, wakasamehewa dhambi zao zote na makosa yao, nao wanangojea wito wao wa kwenda Juu.

28 Nasi tumekuja kuzungumza na kufanya ushirika huu mdogo pamoja na ndugu yetu kabla ya kuondoka kwenda katika nchi za ng'ambo kutekeleza lile agizo kuu: "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Mbariki ndugu yetu mpendwa, Bwana, katika utume wake. Libariki kanisa dogo linalomngojea sasa arudi, likimngojea kwa maombi mchungaji wao mpendwa. Mbariki msaidizi wake atakayepachukua mahali hapo, wazee wote, na hawa watu.

Bariki usomaji wa Maandiko, na sasa utupe ushirika pamoja na Wewe, sasa hivi, kwenye Neno, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

29 Sasa, tukinena juu ya Neno, na neno la *Ushirika*, nikifikiria, nikipanda huko juu, huenda ikawa ni wakati wa ajabu kuzungumza tu juu ya ushirika kwa muda mfupi. Hilo ni moja ya mambo makuu zaidi. Kila mtu anatamani ushirika. Watu siku hizi, watasema, "Je, utakuja tu pamoja nami nyumbani kwa muda mfupi? Hebu tuwe na muda mfupi tu wa ushirika."

30 Halafu, mara nyingi, wafanyabiashara watasema, "Je, utakula chakula cha mchana pamoja nami leo wakati wa mlo wa kutwa?" Ama twende nje tukale chakula kidogo cha mchana pamoja, tule kipande cha sambusa ama chochote kile, wakati wa ushirika: kula. Mlo huendana na ushirika.

31 Na tunapozungumza alasiri ya leo, Roho Mtakatifu wa Mungu na alichukue Neno la Mungu na kulisha kila nafsi yenye njaa hapa ndani. Mlo huambatana na ushirika. "Wala mtu hataishi kwa mkate tu," asema Bwana, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Roho Mtakatifu, basi, anapenda kula na kushirikiana na mwaminio. Ni wakati wa jinsi gani. Sote tumekusanyika kwenye meza kuu sasa, ambapo mambo mazuri ya Mungu yamelundikana tu juu. Mungu anao wingi wa baraka Zake, kila kitu tunachohitaji: vitamini zote, kila kitu tunachohitaji, kutufanya tuwe Wakristo halisi, imara, wenye afya njema, waliojazwa na Roho Wake, wakaoshwa katika Damu Yake, na ni wakati wa jinsi gani tunaoweza kufanya ushirika.

32 Basi umewahi kuwazia, methali ya kale ambayo mtu amewahi kusema (mama yangu alikuwa akiitumia hii sana): "Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba." Hiyo ni kweli. Hebu waangalie. Hutawaona hua na ndege wala mizoga pamoja, kwa sababu hawawezi kula mlo ule ule. Mla mizoga, koho, anaweza kula tu chochote. Kunguru anaweza kuketi huko nje juu ya mzoga na kuula. Hua asingeweza kufanya hivyo. Kama angeula, ungemuua. Kamwe hawezi kuula. Anaingia kwenye shamba la ngano na kuanza kula ngano. Anashirikiana na wa aina yake. Lakini hii hapa sehemu ya kushangaza: Je, ulijua kunguru anaweza kula mzoga na pia kula ngano? Anaweza kula zote mbili, lakini . . . Unaona?

33 Unaona, huna budi kuwaangalia hao jamaa, wa aina hiyo, wanaoweza kuketi mkutanoni na wakijifanya kufurahia mkutano, na kurudi nje na kula mambo ya ulimwengu. Hivyo ndivyo waaminio wa kijamii walivyo siku hizi. Lakini tunapenda kukusanyika pamoja na wale waliojitenga na mambo ya ulimwengu: walioitwa na kufanywa viumbe vipya katika Kristo Yesu, na kushirikiana kwenye baraka za Roho Mtakatifu. Ni jambo la ajabu namna gani.

34 Sasa, mwanadamu alizaliwa apate kuwa na ushirika. Mwanadamu, hapo mwanzo, kule nyuma katika bustani ya Edeni, alikuwa na ushirika wa ajabu. Mungu alishuka na kushirikiana na kundi Lake la wanaume na wanawake kila jioni. Wakati wa jua kupunga, Mungu angeshuka chini ya mitende mikubwa, labda Nuru Yake takatifu, tuseme, ikiwaangazia Adamu na Hawa, katika kanisa kuu huko nje. Ushirika pamoja na Mungu; hawakuwa na hofu yoyote mradi tu walikuwa wakifanya ushirika.

35 Ninapenda ushirika na watu. Ninapenda kutoka na kuzungumza na watu wanaompenda Bwana, na kushirikiana nao, kwa maana tunaona jambo lile lile. Nia zetu ni zile zile. Mawazo yetu ni mamoja. Ninapenda kuongea na watu kwenye . . . Nina rafiki anayeketi papa hapa ambaye anapenda kuwinda na kuvua samaki. Mara nyingi tuna ushirika mwingi pamoja, kuketi tu huku tukiyazungumzia mambo hayo, kwa sababu tunayapenda mambo hayo. Sasa . . .

36 Lakini ushirika mkuu zaidi ambao mtu yeyote aliwahi kuwa nao ni wakati alipokuwa akifanya ushirika na Mungu, wakati Mungu alipojitolea Mwenyewe wazi kwa mwanadamu apate kuendelea kushirikiana na viumbe Wake, Muumba na kiumbe Chake.

37 Sasa, Mungu alipokuwa akishirikiana na Adamu katika bustani ya Edeni, Adamu hakuhangaishwa na chochote. Kila kitu kilikuwa sawa kabisa, na kinaendelea vyema. Haikumbidi kuhofu juu ya nguo zake; haikumbidi kuhofu juu ya chakula. Haikumbidi kuhofu juu ya magonjwa; haikumbidi kuhofu juu

ya mauti, huzuni. Hakujua chochote juu yao, uhuru tu kama wa mtoto. Alikuwa na Baba wa Mbinguni ambaye alimwangalia na kushiriki pamoja naye kila siku. Si lingekuwa ni jambo zuri sana kama tungeweza kurudi hivyo tena?

38 Na mnajua kila mtu aliyekombolewa leo hii, kwamba anaishi pungufu ya majaliwa yao ya ushirika wa namna hiyo pamoja na Mungu? Unaamini hilo? Mungu atashughulika na kutupa kila kitu tunachohitaji katika safari hii. Na mwishoni mwa kumalizikia kwa maskani hii ya kale ipatikanayo na mauti, Mungu ameahidi kutupa nyingine. Amina.

39 Unajua nina wazo dogo la kuchekesha kuhusu tunapokufa. Afadhali nilielezee; nipo nyumbani. Ndugu Joseph alisema wakati mmoja . . . Nilikuwa ninataka kujibu swali la mwanamke mmoja ambalo linaweza kuwa kinyume kidogo. Akasema, "Ndugu Branham . . ."

Nikasema, "Sasa, Ndugu Joseph, hili hapa ninalotaka kusema, na kwa- . . ."

40 Akasema, "Angalia, usiliseme." Kasema, "Tulipoandika ninii . . . sheria zetu na kile tunachoamini katika kanisa hili, tunamalizia na koma, sio nukta. Tunaamini hili, pamoja na mengi zaidi tunayoweza kusikia." Kwa hivyo hi—hilo ni zuri sana; napenda hilo.

41 Sasa, wakati . . . Yohana 14, wakati aliposema, "Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi," akizungumza na wanafunzi Wake kabla ya kuondoka, siwezi kuwazia hayo kuwa ni ya mawe na matofali na saruji. Ninaamini maskani aliyokuwa akizungumzia ilikuwa ni mwili mwingine wa kuishia. Mnaona? "Nyumbani mwa Baba yangu kuna maskani nyingi ama makao mengi. Iharibuni maskani hii, nami nitaisimamisha katika siku tatu." Na tena, "Maskani hii iliyo ya kidunia hii ikiharibiwa, tunayo moja iliyokwisha kutayarishwa na inangoja." Mnaona? Basi ninaamini, kwamba wakati sisi . . .

42 Nilikuwa nimesimama siku chache zilizopita kwenye Mlima Wilson, Palomar, hasa, huko California, chumba kile kikuu cha uangalizi, ambapo unaona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga ya nuru, nao walikuwa wakipima muda. Na jinsi sayansi inavyogeuka-geuka katika theolojia yao, nawaambia. Nilipoenda shuleni, na kuisikiliza sayansi hiyo, nitawaambia, hakuna kitu kama ile niliyofundishwa shuleni.

Mnajua, baba yangu alizoea kuketi chini, naye akasema (kwa Biblia), akasema, "Billy, inawezekanaje kamwe . . ."

Nikasema, "Baba, jua linasimama kikamilifu kabisa, thibitisho la kisayansi, nayo dunia inalizunguka."

Akasema, "Yoshua alisema alisimamisha jua."

Nikasema, “Utafanyaje hilo?” Nikasema, “Baba, tunafundishwa shuleni.” Nami nikasema, “Wamelithibitisha kisayansi.”

Akasema, “Vema, labda wamelithibitisha, lakini hiyo—hiyo si sayansi ya aina yangu,” akasema. Aliamini, kasema, “Yoshua . . . ”

43 Nami nilimwuliza mwalimu wa Biblia shuleni. Akasema, “Vema, bila shaka, unajua, Yoshua, hao watu katika siku hizo walikuwa wajinga, ndipo Mungu akaangalia tu ujinga wake, naye akaisimamisha dunia badala yake.” Lakini sasa, hawana budi kulighairi hilo. Jua huzunguka. Jua huzunguka pia. Wamelithibitisha kisayansi. Jua huzunguka.

44 Nilipokuwa mvulana nikienda shuleni, walisema jua linapotua, huzimulika nyota, na halafu nyota zinazoakisi mwanga wa jua. Sasa, wamethibitisha kisayansi kwamba hilo haliwezekani. Inachukua mabilioni na mabilioni ya miaka kwa nuru ya jua, ikisafiri maili milioni kadhaa kwa saa, chochote kile, ikisafiri kutoka kwa jua, kufikia moja ya hizo nyota, kwa hiyo sivyo. Nyota hutengeneza nuru yake yenyewe sasa.

45 Mvulana wa Ndugu Moore alihitimu, ndipo mmoja wa wanasayansi wakuu akaja, hapa majuma machache yaliyopita, akamkumbatia, na kumpa udhamini wake. Akasema, huko Washington, DC, wana vitabu mia moja na ishirini na vinne vya hivi karibuni sana vya wanasayansi juu ya sayansi yote ya kisasa ambayo imethibitishwa kisayansi. Kasema, “Ewe kijana mwanamume, itakuchukua miaka miwili kusoma kitabu hicho. Nawe ukiisha kuvisoma itabidi utupilie mbali kila kitu ulichojifunza, kwa maana kutakuwa na kitu tofauti.”

46 Basi aliposema hivyo, niliitikia “Amina” kidogo, huko nyuma. “Lakini . . . ” nikawazia, ningeweza kusimama na kusema hivi: “Lakini ninacho Kitabu hapa ambacho nyakati zitapita na kupita na kupita, kamwe haitakulazimu kuridhiana. Siku zote kitakuwa vile vile, kwa sababu kimevuviwa.” Hawana budi kurejea Kwake kila wakati. Loo, usijaribu kusoma, kufanya nywele zako zipate mvi ukijaribu kusoma sayansi. Soma tu Biblia ya Mungu, maana Ndiyo Kitabu safi kuliko vyote.

47 Basi nafikiri kwamba wakati wowote roho hii inapouacha mwili, tunaingia kwenye nyumba nyingine isiyotengenezwa kwa mikono. Tunaingia katika Uwepo wa Mungu, na huko tunafanya maskani pamoja Naye katika Uwepo wa Bwana Yesu, na huyo ni mweza yote, loo, namaanisha mjua yote, anayeenea kila mahali. Na basi, kama ndivyo Yeye alivyo, ndivyo nasi pia, tutakapoingia kwenye maskani yetu mpya huko. Halafu basi, kama Yeye alisema, “Popote wawili watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao,” basi Yeye hana budi kuwa hapa alasiri ya leo. Kwa hakika tu kama kulivyo na—na Mbingu na nchi,

Yesu Kristo yupo sasa. Lakini jambo ni kwamba, Yeye yuko katika hali ya kutoonekana. Hatuwezi kumwona, lakini kuna kitu fulani kuhusu nafsi ya Kikristo, ambapo mtu anapotambua wakati Uwepo Wake upo, anasimama katika Uwepo wa kitu Fulani ambacho hawezi kukiona.

48 Tunajua kuwa kuna redio inayopitia hapa sasa. Kuna televisheni inayopitia hapa sasa. Macho yetu hayawezi kuishika. Lakini iko katika ulimwengu mwingine; na vivyo hivyo Malaika wa Mungu wamewekwa pande zote kwenye chumba hiki wakiangalia alasiri ya leo. "Malaika wa Mungu wamefanya kituo kuwazunguka wale wamchao." Yesu yuko kabisa, wakati wote, akituangalia. Nasi tunajua kwamba hiyo ni kweli.

49 Ninawazia wakati Eliya, kule chini Dothani, wakati yule Gehazi alipotoka na kutazama kule, na kusema, "Loo, jeshi lote la Shamu, hebu waangalie; wameuzunguka mji huu na tumezingirwa."

Eliya akasema, "Kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao."

Akasema, "Vema, nisingeweza kuona mtu yeyote."

50 Kasema, "Mungu, yafumbue macho ya mvulana huyu." Ndipo macho yake yalipofumbuliwa, milima ilikuwa ikiwaka moto, na Malaika wa moto, magari ya farasi ya moto. Hakika. Yeye yuko hapa.

51 Na wakati Wakristo waaminio wanaweza kuamini kwamba sasa hivi, sasa hivi, tumeketi pamoja, tumeketi hapa katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, katika Kristo Yesu, tukifanya ushirika (Amina.) kwenye Neno la Mungu, Roho Mtakatifu hapa akilichukua Neno la Mungu kwa ono, akiliingiza ndani ya kila moyo namna *hiyo*, Neno linapoendelea na kila mwaminio akilipokea. Loo, laiti tungelisimama na kudai majaliwa yetu tuliyopewa na Mungu. Huo ndio wakati ambapo Mungu anaweza kuuondoa ule mfupa dhaifu kutoka kwa mgongo wa mtu na kuingiza uti wa mgongo halisi wa Injili ya mtindo wa kale ndani yake, mtu atakayeitetea ile kweli, haidhuru inaonekana kuna giza jinsi gani.

52 Mungu aliwaachilia wale wana wa Kiebrania waingie moja kwa moja katika tanuru ya moto kabla hajafanya chochote. Yeye yuko sikuzote; msiogope. Yeye yupo sikuzote. Amina. Basi ikiwa hatua za mwenye haki zinaamriwa na Bwana, tuogope nini? Mungu akiwa upande wako, ni nani anayeweza kuwa kinyume chako? Loo, jamani, liwazieni hilo. Loo, kama Mungu aliruhusu sehemu Zake za Mbinguni kutukusanya pamoja katika mkutano. . . Amina. Jaribu tu kutafuta tundu hilo la kutokea wakati Roho Mtakatifu akilichukua Neno na kulitwanga kama nyundo ya hewa dhidi ya mwamba. Loo, jamani. Akiivunja mioyo yetu ya mawe na kuondoa imani. . .

kutokuamini huko, na kushiriki kwenye Neno. Ushirika ni mzuri sana.

53 Adamu na Hawa walipojitenga na Mungu kwa dhambi, ikawatenganisha, walifanyika wazururaji basi, hawana ushirika, wakitanga-tanga, wakidhoofika. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Dhambi imewatengisha watu na ushirika wa namna hiyo. Siku hizi tunashangaa jinsi tutakavyofanya *hili*, na tunashangaa jinsi tutakavyofanya *lile*.

54 Yesu alisema, "Wapagani hutafuta mambo kama hayo, jinsi sisi. . .tule nini na tuvae nini, ama tutafanya nini na *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Mambo hayo yote," alisema, "watu wa Mataifa, wasioamini, huyatafuta. Lakini Baba yenu wa Mbinguni anajua mnachohitaji hata kabla hujamwomba." Ni hali ya kutojali jinsi gani sasa.

55 Mbona, nina msichana mdogo mwenye macho ya kahawia pale chini, mbona, angeruka uani, chini, au chochote kile; hana wasiwasi, maadamu nimesimama pale. Alisema, "Baba nichukue." Anaenda kucheza. Hana wasiwasi. Nikawazia, "Ee Mungu, laiti ningalikuwa tu namna hiyo, bila wasiwasi kabisa."

56 Siku chache zilizopita, Ndugu Joseph alinitia moyo sana. Niliona mambo mengi sana yakiinuka makanisani ambayo hayafai kuwako, na loo, vema, nilikuwa Mwairishi mnajua, ilinibidi nitoke nikayakomeshe mwenyewe. Nami ni—nilikuwa nitoke nje na kusema, "*Hili* haliwezi kuwa *hivi*, na *hili* haliwezi kuwa *hivyo*: hamwezi kufanya hivyo, kwa sababu mtauharibu mpango wa Mungu. Mnaingiza mambo mle ambayo hayafai kuwako, na yote haya." Nami nilijua lilikuwa ni kosa, ni kosa Kimaandiko. Nami . . .

57 Muda si muda mwajua nikaanza kujikuta kidogo nimetoka mstarini, nikiingiwa na uchungu. Nilisimama huko nje nikaenda, nikaanza kuomba, ndipo Joseph akashuka akaja. Akasema, "Tazama, nimesoma historia ya Martin Luther hivi punde, na swali lilikuwa ya kwamba hawakushangaa kuhusu Martin Luther kuweza kulipinga kanisa Katoliki na kuponyoka. Lakini kilichoshangaza kwa Martin Luther, ni ule ulokole wote uliofuata, naye akainuka juu kutoka katika hayo yote. Hilo ndilo jambo kuu."

58 Kisha nikasikia tuseme, kwamba Kristo alisema, "Hiyo ni nini kwako? Nifuate Mimi. Nitayashughulikia hayo mengine. Wewe endelea mbele tu na unifuate Mimi." Hivyo ndivyo ilivyo. Kisha urudi kwenye hali ya kutokuwa na wasiwasi tena, vema.

59 Mwanadamu alipojitenga na Mungu, aligeuka akawa mzururaji, akitanga-tanga kila mahali. Na hiyo ni picha ya jinsi gani siku hizi. Mwanadamu anapotoka kabisa kwenye ushirika pamoja na Mungu; juma hili yeye ni Mmethodisti, juma lijalo ni Mbaptisti, halafu yeye ni *hili*, na *lile*, na *linginelo*: akitanga-tanga, akichukuliwa na kila upepo wa mafundisho. Moyo

unapaswa kuimarishwa. Sisemi unapaswa kuwa Mmethodisti, Mbaptisti, ama chochote kile; unapaswa kuwa sawa na Mungu.

60 Hapo. Haijalishi unaenda kanisa gani, wapi . . . kikundi. Wewe shiriki na kundi lolote, kama ni Assemblies, au Umoja, au Uwili, au Watakatifu wa Siku za Uso- . . . Mvua, ama chochote kile, mradi tu ushirika wako ni safi kwa Mungu. Amina. Biblia ilisema, sisi . . . "Damu ya Yesu Kristo hutusafisha na dhambi zote, ndipo tunakuwa na ushirika sisi kwa sisi." Amina. Napenda hilo. Loo, jamani. Njia . . .

61 Ndipo Mungu akamwona mtu huyo nje ya ushirika, basi lazima afanye jambo fulani ili kukirudisha kiumbe Chake mahali ambapo angeweza kupata moyo wake tena, ambapo angeweza kupata njia ya—yake ya kurudi. Sasa, hapo ndipo se—sehemu ya huzuni inapoanzia sasa hivi.

62 Sasa, mwanadamu amejaribu kuweka kitu fulani badala ya ushirika tangu mwanzo wa wakati. Sasa, siku hizi tunasema, "Hakika, kila mtu aje ajiunge na kanisa letu. Tunayo." Methodisti wanataka kuamini hilo kuhusu lao, Baptisti kuhusu lao, Katoliki kuhusu lao, Presbiteri kuhusu lao, Pentekoste kuhusu lao, la Kimitume kuhusu lao. Na katika hilo walifanya azimio la kanuni za imani. Nao wameanzisha kanisa hili na lundo la kanuni za imani, na katika hilo wanadai kwamba *hiyo* ndiyo njia ya kufanya ushirika. Sikilizeni, huwezi kufanya ushirika kwa njia hiyo. Ungeweza kujiunga na kila kanisa lililoko nchini na bado usiwe na ushirika pamoja na Kristo. Mungu aliweka mpango wa pekee kule nyuma, pale mwanzo, wakati alipomchinja mwana-kondoo, ama kondoo, kisha akatandaza mkeka wa kuwakaribisha wanadamu tena kwenye ushirika, nao ulikuwa ni kwa njia ya damu. Amina.

63 Sasa, unasikia machache sana kuhusu Damu siku hizi. Daima tunazungumza juu ya mambo mengine. Tunazungumza juu ya nyakati na juu ya bomu la atomiki. Mambo hayo ni sawa, lakini, ndugu, kwangu mimi bila kumwagwa kwa Damu hakuna ondoleo la dhambi. Na wakati Damu imewekwa kazini ipasavyo, dhambi imeondolewa, basi mwanadamu anarudi katika ushirika na Mungu. Amina. Tunachohitaji leo ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale, ulionunuliwa kwa Damu. Amina. Uhai uko kwenye mkondo wa damu. Na wakati Damu ya Kristo inapotusafisha na udhalimu wote, basi tunao ushirika pamoja na Mungu.

64 Unaweza kutubu, au kuja na kufanya maungamo, uende kwenye majaribio ya miezi sita, unyunyiziwe kwa kidau cha chumvi, na kuwa mfuasi wa kanisa la Methodisti (Naam, bwana.), na kufanya ushirika na kila mmoja wao. Hiyo ni kweli. Au unaweza kuja kupitia kanisa la Kibaptisti, na kupata mkono wa kuume wa ushirika, na kufanya maungamo, na kubatizwa katika maji, upate ushirika kwa kanisa la Kibaptisti. Hebu

nikwambie, katika kanisa la Kipentekoste unaweza kuomba kwa muda kidogo mpaka unene kwa lugha, na kufanya ushirika na kila mmoja wao. Lakini, ndugu yangu, dada, mpaka nafsi yako itakapooshwa katika Damu ya Yesu Kristo, hutawahi kuwa na ushirika na Yeye. Kweli.

65 Na wakati roho yako imeoshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo, uovu wote, chuki, husuda, ugomvi, mambo haya yote yamekufa. Damu hufanya upatanisho. Amina. Hiyo ndiyo sababu siku hizi katika ushirika wetu wa Kipentekoste, katika ushirika wetu mbalimbali wa full-Gospel, tuna makelele mengi sana, ninii nyingi sana . . . tofauti na kadhalika katika kundi letu, kwa sababu "itikadi" ze—ze—zetu mbalimbali na kadhalika, hasa, zimeingia. Ni kwa sababu mmoja atajiondoa na kuwa *hivi*, na huyo mwingine ajitoe na kuwa *hivi*, na mwingine ajiondoe na kuanzisha dhe—dhehebu au shirika. Sababu yenyewe ya hilo ni kwa kuwa kwanza kabisa moyo wa mtu huyo haukuwa sawa na Mungu. Mungu anatutaka sisi sote tuwe Mwili mmoja: Mwili mmoja wa waaminio, waliobatizwa katika Roho Mtakatifu. Amina. Loo, jamani, Mungu aliweka mkeka mmoja wa kukutana na watu. Huo ulikuwa mkeka wa makaribisho. Kutoka kwa ule ushirika uliokuwa umeanguka wakati mmoja, kurejeshwa ni ile Damu. Kupitia Damu unao ushirika, kule kurudishwa kwa ushirika pamoja na Mungu.

66 Adamu hangeweza kukutana juu ya theolojia yake mwenyewe. Alijishonea majani ya mtini akajizungushia, lakini hayangefaa kitu. Aliunda shirika lake mwenyewe; akajitengenezea dhehebu lake mwenyewe, lakini halingefaulu.

67 Na leo hii, loo, nilipoendesha gari kando ya jamii yenu ya wakaa uchi chini hapa, iko barabarani hapa juu. Hata hawawezi kungoja mpaka—mpaka jua liwe joto. Wamelala uchi ufukoni huko chini; wanaume na wanawake pamoja, walionekana kama kundi la sijui-ni-nini. Na kila mmoja wao, labda, akiwa mfuasi wa kanisa fulani mahali fulani, akikariri sala chache pale kwa shanga, ama kuimba Doksolojia mahali fulani, labda katika kwaya, na kulala nje namna hiyo. Inaonyesha kwamba kitu fulani kimeachilia. Viumbe wenye maadili, watu wenye busara wasingefanya hivyo. Ndugu, hiyo ni kweli. Ukiwahi kupata mguso wa Kristo moyoni mwako, utakaa mbali na sehemu kama hizo. Amina. Sasa, naam, hiyo inaweza kutokubaliana . . . unaweza usikubaliane na hilo, lakini ingia ndani ya moyo huo vizuri wakati mmoja, uone kile Mungu atafanya juu yake.

68 Nakwambia, hata maskini msichana wangu, ana umri wa miaka miwili tu, alitoka chumbani pale . . . nje katika . . . hivi majuzi, nje kwenye kitalu, basi kulikuwa na mwanamke huko nje aliyekuwa akikata nyasi huku amevaa maskini nguo fu—fupi sana iliyoonekana mbaya sana, naye mtoto huyo wa miaka miwili akaingia na kusema, "Loo, Baba, yule mwanamke

alisahau sketi yake." Sasa, haya basi. Mnaona, mtoto mchanga anajua vizuri zaidi.

69 Lakini wakati wanaume na wanawake wanaporuhusu mioyo yao ichomwe moto, ni mashetani, nguvu za ibilisi. Hakukuwako ila na kitu kimoja tu katika wakati wote ambacho kingewavua watu nguo, nacho kilikuwa ni mashetani, kuwavua wanawake nguo, hasa (Hiyo ni kweli kabisa.), ama wanaume, mojawapo. Inaonekana kama kundi la wanyama wa kabla ya historia, wamelala huko nje wamevuliwa nguo bila dhamiri. Biblia ilisema wangechomwa dhamiri zao kwa chuma cha moto.

70 Na watu hao hao, huyu ninayemzungumzia hasa, nimjuaye sasa, anaimba katika kwaya. Loo, jamani. Wana ushirika na makundi yao, hakika. Lakini, ushirika pamoja na Kristo. Naam, bwana.

71 Ninajua hilo ni kali, ndugu, dada. Lakini Mungu atusaidie. Kama kanisa la Kipentekoste halitarudi kwenye Damu ya Kristo tena, mmekwisha. Hiyo ni kweli. Rudini. Ilikuwa ni dha—dhambi zamani za kale kwa Wapentekoste kutenda hivyo. Hawakufanya hivyo muda mrefu uliopita. Lakini wanafanya hivyo pia, sasa, ni kwa sababu mimbara inalegea.

72 Unaanza kufikiria kuwa wewe ni mfuasi wa kanisa *hili*, ama dhehebu, ama *kitu kingine* kama hicho. Afadhali uwe na ushirika tena pamoja na Kristo. Amina. Litakuwa jambo la kutisha moja ya siku hizi, moja ya masikitiko Hukumuni. Mwuza pombe haramu hatasikitika; anajua hukumu yake ni gani. Mwongo na mwizi, wanajua hukumu yao ni nini wakisimama mbele za Mungu. Lakini wakati masikitiko yatakapokuja, ni kwa wafuasi wa makanisa ya Kipentekoste watakaowekwa upande mmoja, kwani walijua vyema na kwa makusudi wakaingia humo. Amina. Haleluya!

73 Tunachohitaji siku hizi ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale, unaotikisa. Hebu na turudi mahali pake tena chini ya Damu ya Bwana Yesu, chini ya ushirika.

74 Imekuwa njia ya kukaribia sikuzote kote katika wakati, kote kupitia kwa watu. Tazama jinsi ilivyokuwa, njia pekee ya Mungu. Kitabu cha kale zaidi katika Biblia ni Ayubu. Ayubu alipomkaribia Mungu na akafanya ushirika pamoja na Mungu kupitia damu iliyomwagika, Ayubu alitoa mwana-kondoo kila wakati alipoenda kwenye ushirika. Waabuduo wa Agano la Kale, kote kote kutoka Mwanzo hadi kwenye Agano Jipya, kila wakati wangeenda kufanya ushirika na Mungu, wangetoa sadaka ya kuteketezwa, wamchinje mwana-kondoo kwanza, kwa sababu wanakaribia chini ya damu.

75 Ayubu, wakati alipokuwa. . .alipomkaribia Mungu, angemchinja mwana-kondoo. Hicho ndicho Kitabu cha kale zaidi katika Biblia, kilichoandikwa kabla Mwanzo hakijaandikwa. Musa aliandika Mwanzo, sasa, mamia ya

miaka baadaye. Lakini angalia, Ayubu kilikuwa ndicho Kitabu cha kale zaidi, na kote kutoka Edeni, Ayubu angetoa dhabihu, amwage damu ya mwana-kondoo, na kupitia kwa damu hiyo angekiri kosa lake: "Mungu na anirehemu sasa, nami nakukaribia Wewe kwa damu."

76 Mnajua ni kwa nini watu hawajibiwi maombi yao jinsi ipasavyo? Wanakuja katika harakati za kisaikolojia badala ya kwa njia ya Damu. Hiyo ni kweli. Njoni kwa Damu.

> Mwana-Kondoo mpendwa anayekufa, Damu
> Yako ya thamani
> Kamwe haitapoteza nguvu zake,
> Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
> Litakapookolewa, lisitende dhambi tena.

77 Hicho ndicho hatuna budi kupitia: Damu iliyomwagika. Na hapo Ayubu alitoa damu iliyomwagika alipomkaribia Yehova, akijua ya kwamba Mungu hatampokea kwa kitu kingine chochote. Ukimkaribia leo kwa jina la mtu mwema, "Ninalipa madeni yangu. Siidanganyi serikali. Ninalipa ushuru wangu wa mapato. Ninafanya mambo haya yote. Mimi ni jirani mwema," hata hivyo, Mungu hatakusikia kamwe. Ukisema, "Mimi ni mshiriki mwaminifu wa kanisa, natoa zaka ya pesa zangu, nilitoa matoleo makubwa kanisani, mimi ni nguzo kule," Mungu hatakupokea kamwe, kamwe, hata kidogo.

78 Ukisema, "Vema, mama yangu alikuwa mwanamke mzuri; baba yangu alikuwa mtu mzuri; babu yangu alikuwa mhubiri. Yote hayo ninafanya wala sijawahi kufanya *hivi*; sijawahi kuiba; sinywi pombe; sivuti sigara; sisemi uwongo; sifanyi mambo haya kamwe." Mungu kamwe hatakusikia.

79 Na haidhuru wewe ni nani, umekuwa mbaya jinsi gani, kama utakuja kwa njia iliyowekwa na Mungu kupitia Damu ya dhabihu, ukichukua na kuweka mkono wako juu ya kichwa cha Mwana-Kondoo aliyekufa, cha Mwana-Kondoo anayekufa, na kukiri makosa yako, na kumkubali, basi Mungu ataijaza nafsi yako na Roho Mtakatifu, akiteketeza na kuondolea mbali uovu wote, tamaa za mwili, na kukufanya kuwa kiumbe kipya.

80 Ayubu, namwazia Ayubu siku hiyo kama baba. Alikuwa na watoto kadhaa. Kidogo walikuwa wakaidi. Naye sikuzote alikuwa akiwafikiria watoto wake. Je, haingekuwa bora zaidi iwapo washiriki wote wa kanisa la Chicago wangekuwa na wazo kama hilo kuhusu watoto wao? Msingekuwa na uhalifu wa vijana. Msingeona ghasia hizi za ubaguzi wa rangi, na, ninamaanisha, ghasia hizi na mambo waliyo nayo hapa siku hizi: kurushiana risasi, mauaji, wizi, ubakaji, na mambo haya yote, ni kwa sababu watu hawawajali watoto wao. Jambo la kwanza wanalosema, "Vema, niliwapa malezi walipokuwa wadogo, yaliyosalia nikamwachia mwalimu wa shule ya Jumapili," naye yuko huko nje kwenye dansi, labda, usiku kucha, anaingia, huku

amevaa kama namna fulani, anaenda kwenye sarakasi badala ya kanisa. Na kuwaweka watoto wako mikononi mwa kitu kama hicho? Mama, jionee aibu!

81 Unapaswa kumweka mtoto huyo aliye na mahitaji *huko* chini na kusoma Biblia. Weka mikono yako juu ya vichwa vyao, ukamwite Mungu. “Mungu, uturehemu. Mwokoe binti yangu, mwanangu.” Naam.

82 Ninapenda kufanya hivyo, kuwachukua hao wasichana wangu wadogo, naam, niwaketishe pale chini, nao wanaketi, macho yao madogo yakisikiliza, ama—ama masikio yao yakisikiliza, na macho yao yakitazama, nitawaambia kuhusu, yote kuhusu Yesu, na jinsi Yeye anavyowapenda, na kadhalika. Watapiga magoti kuzunguka viti na kuomba kama tu sisi wengine. Hivyo ndivyo tunavyotaka kulifanya, sivyo? Hivyo ndivyo wengi wenu wanavyofanya. Hilo ndilo unalopaswa kufanya.

83 Nilienda katika makazi mengi, nao watoto wote sikuzote wamekusanyika kwa maombi ya familia. Mungu, ibariki familia hiyo. Hicho ndicho kifungo kifungacho. Kama ulifanya hivyo nyumbani kwako, hakungekuwako na kesi nyingi hivi za talaka, na mambo yakiendelea jinsi yanavyoendelea. Mnafanya ushirika nyinyi kwa nyinyi.

84 Kisha ninamwona Ayubu, watoto wake walifunga ndoa wakaenda njia tofauti tofauti, kama wanavyofanya kama ndege kutoka kwenye kiota. Ayubu, akijua ya kwamba hakukuwako na njia nyingine, hakuna uwezekano, kwamba mwanadamu angeweza kumkaribia Mungu na kufanya ushirika Naye, ila tu kupitia kwa mwana-kondoo wa dhabihu, kwa njia ya damu; Ayubu alisema, “Labda watoto wangu wanaweza kuwa wametenda dhambi, kwa hiyo nitatoa mwana-kondoo kwa ajili yao.” Kitu fulani kilimwambia Ayubu ni heri ajitayarishe, heri ajitayarishe. Na ndipo alipotoa sadaka ya mwana-kondoo wa dhabihu kwa ajili ya watoto wake, siku moja ilitukia. Dhoruba zilikuja na kuwaua wengi wao, na moto na kadhalika, na uharibifu. Lakini kabla haya hayajatokea, Ayubu alihakikisha kwamba kila mmoja alikuwa chini ya damu. Amina.

85 Kukataliwa, wamemkataa leo. Taifa hili linamwua Kristo haraka iwezekanavyo, likimhuzunisha Roho Mtakatifu kwa kanuni za imani na taratibu za dini, wakimhuzunisha Roho Mtakatifu.

86 Nilikuwa nikisoma si muda mrefu uliopita. . .Nilisikia mahali fulani, juu ya mwinjilisti huyu mashuhuri Billy Graham alipokuwa Scotland. Mnajua kuna shida gani? Kama Wapentekoste wangeweka vichwa vyao pamoja, badala ya kuvunjika na kufanya kila kitu kama mfanyavyo, ibada zenu zingekuwa zikiendelea kama za Wabaptisti; lakini Wabaptisti waliwanyang’anya. Hiyo ni kweli. Wana uamsho, wanaenda

mahali fulani, kwa sababu walitupa kila kitu walichokuwa nacho juu ya madhabahu, nabii wao, nao wakaenda zao. Wanakaa nyuma yake. Lakini siku hizi, hebu mmoja ainuke kutoka kwa Assemblies, na . . .?. . .

87 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .linaketi kama elfu saba, nami nilikuwa na yapata elfu saba wamesimama nje, naye alikuwa na yapata elfu tatu. Hebu tubadilishane. Kwa hivyo nilipoenda kule kumwona, nilidhani maskini mvulana fulani mdogo atakuwa amesimama hivyo, akikariri shairi, shairi la watoto: "Yesu, Mtoto mdogo aliyezaliwa horini." Lakini nilipomwona mvulana huyo mdogo, aha, ilikuwa ni tofauti. Jamaa huyo mdogo karibu tu urefu *huo*, sikujua hata alikuwa ni mtoto David. Alitupa koti lake, akachukua somo, na kuhubiri kama mhubiri. Namaanisha Mungu alikuwa pamoja naye.

88 Nikasema, "Huyo hapo mvulana mdogo ambaye Mungu alimtuma. Sasa, kama ninyi kina baba wa kanisa mtamzingira, msimwache ashikwe na majivuno kichwani mwake, na kumwacha aende kombo na lundo la fedha, na mumzingire, na kuweka ushawishi mzuri juu yake, atawaokoa maelfu ya watoto wadogo."

89 Lakini nilikuwa nimesimama kule Oregon, Grants Pass, Oregon, asubuhi moja, mbele ya Ndugu Hall na hao wengine. Nikasema, "Tazama. Halitafanikiwa." Nikaliambia baadhi ya hilo kundi, nikasema, "Vipi kuhusu kumleta maskini David sasa aje katika mji kama huo afanyavyo?"

"Mbona," kasema, "Yeye ni wa Umoja."

90 Nikasema, "Sijali kile alicho. Mungu yu pamoja naye." Vema, bila shaka, sasa ilibidi Assemblies kujipatia David kadogoo. Nalo Church of God likajipatia David kadogoo. Basi muda si muda mnajua, kuna maelfu ya akina David kadogoo. Kanuni yenyewe ambayo Mungu alikuwa akijaribu kuwaletea watoto, wakakirarua kitu hicho.

91 Hawaijui siku yao. "Maksai anajua hori la bwana wake, na nyumbu anajua zizi lake, lakini watu Wangu hawajui," kasema Mungu. Hiyo ni kweli. Hawajui siku ya kujiliwa kwao. Ni jambo la kuchekesha zaidi kujaribu, au, jambo la ajabu zaidi kuwafanya watu wa Mungu waone siku ya kujiliwa kwao. Bila shaka wanaanza tu kuvuta *kitu kingine*, au hulka au *kitu fulani*, wala hawajui jinsi ya kukishughulikia. Wanauhamisha ushirika wao kwenye dhehebu badala ya kuuingiza katika Kristo.

92 Ndipo Ayubu alipoona yale aliyokuwa amefanya, basi, jinsi ambavyo alikuwa ametoa dhabihu hiyo, Biblia ilisema kwamba watoto wake walikusanyika pamoja naye. Sasa, kufanya maandalizi.

93 Wazo lingine: Israeli, walipokuwa na ushirika, angalieni walichofanya. Kabla ya kuja kwa yale maangamizi makuu, yule malaika aliyeziangamiza nchi zao, yule malaika wa

kuangamiza, jambo la kwanza lililotukia, Israeli waliamriwa kumchukua mwana-kondoo, na kumchinja, na kupaka damu juu ya mlango. Na kila familia iingie na kumla huyo mwana-kondoo: kufanya ushirika kwenye mwana-kondoo aliyechomwa. Kula mwili wa dhabihu iliyokufa kwa niaba yao. Mungu alisema, "Nitakapoiona hiyo damu, nitapita juu yenu." Malaika wa mauti asingeweza kuwagusa, kwa sababu damu ya mwana-kondoo ilikuwa juu ya mlango, nao walikuwa hapa ndani wakiwa na ushirika, wakifanya ushirika kumzunguka mwana-kondoo. Ndivyo ilivyo mioyoni mwetu tunapotumia Damu ya Bwana Yesu kuondoa dhambi zote, ndipo tunaweza kuwa na ushirika wa kula Neno la Mungu kwenye meza ya Mungu, tukishiriki mambo ya kitauwa.

94 Ukihubiri uponyaji wa Kiungu, kila mmoja wao katika Kristo anasema, "Amina, hiyo ni kweli." Ukihubiri kwamba inatupasa kuweka kando dhambi zote, kijicho, ugomvi, na kadhalika. "Amina," anasema mwaminio wa kweli, "hiyo ni kweli." Kushiriki katika Neno, mnaona ninachomaanisha?

95 Sasa, sasa, daima, mahali pekee ambapo Mungu amewahi kukutana, aliposema ya kwamba angewahi kukutana na mwanadamu. . . Kamwe hakuahidi kukutana nasi katika madhehebu. Kamwe hakuahidi kukutana nasi kwa njia nyingine yoyote, bali kupitia damu iliyomwagika. Israeli wa Agano la Kale, haijalishi walikuwa wapi, wao, kabla hawajamwabudu Mungu, walifika mahali pa kawaida pa kukutania, ambapo palikuwa ni ile maskani nyikani. Kila mtu angepanda kilele cha kilima, naye alitaka kushirikiana na Mungu, aliingia kwenye ile maskani nyikani, huko apate kukutana na Mungu. Musa, Miriamu alipopigwa na ukoma, aliingia na kuanguka mbele za Mungu chini ya damu iliyomwagika. Mnaona?

96 Jiweke kibinafsi mahali pafaapo, sasa, usiku wa leo, unaona; ingia chini ya Damu. Mambo haya yote yaliyo moyoni mwako, yaondoshe. Nenda mbele za Mungu chini ya Damu, ukikiri makosa yako, kisha uite, na urekebishe, "Nisaidie."

97 Musa alipata jibu la maombi mara moja kwa sababu alipitia njia ya Mungu, chini ya damu. Kabla hajaweza kufanya ushirika; aliingia chini ya damu. Sasa, angalieni, mwana-kondoo alichinjwa.

98 Huko nyuma katika Agano la Kale walikuwa na ndama mwekundu. Alimwambia Musa walipoanza safari yao, akasema: "Sasa, fanya maandalizi kwa ajili ya utakaso wa watu wanaposafiri, kwa maana wakifanya makosa, wametoka kwenye ushirika. Na kabla ya kuweza kufanya ushirika, nataka uwaandalie maji ya farakano." Ndipo Musa akaamriwa: chukua ndama mwekundu, ndama mchanga.

99 Sasa, nataka mtambue neno *nyekundu* linamaanisha jambo fulani. Kwangu na kwenu, *nyekundu* linamaanisha "hatari."

Lakini *nyekundu* katika Biblia linamaanisha "ukombozi," ukombozi kwa njia ya damu. Kote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo ni mkondo mwekundu wa damu kotekote, mwekundu kote kote. Angalieni, iliwabidi waingie chini ya damu iliyomwagika.

100 Sasa, Yeye alisema, "Chukua ndama mwekundu." Sasa, umewahi kuona kisayansi? Ukichukua kitu chekundu kabisa, na kuangalia kupitia nyekundu kwa nyekundu, basi inaonekana nyeupe. Je, umewahi kujua hilo? Nyekundu kupitia kwa nyekundu inaonekana nyeupe. Na kwa hiyo Mungu, akijua ya kwamba mwanadamu asili yake ilikuwa ni mwenye dhambi, akijua ya kwamba kwanza kabisa alikuwa mkosaji, alifanya maandalizi ya Damu iliyomwagika. Naye Mungu, akiangalia kupitia Damu ya Bwana Yesu, anakuona wewe mwenye dhambi mwekundu ukiwa mweupe kama theluji. Huna dhambi tena. Mungu anapoangalia kupitia kwa Damu ya Kristo, haijalishi umefanya nini, umetenda dhambi kiasi gani, umefanya nini, kama Damu ya Kristo imepakwa moyoni mwako, Mungu anakuona mkamilifu.

101 Sikiliza. Nitawaambia siri ndogo katika dakika chache kuhusu uponyaji wa Kiungu na kuhusu mambo. Jambo la kwanza, marafiki, ni maandalizi ya moyo wa mwanadamu. Naam, bwana.

102 Hapa, siku chache zilizopita, nilikuwa huku juu Chicago, ambako sayansi ya kale ilizoea kusema, "'Mwanadamu hufikiri kwa moyo wake;' upuuzi, ati Biblia imekosea. Hakuna uwezo wa kiakili moyoni wa kufikiria. Mtu hufikiri kwa kichwa chake, kwa akili yake." Lakini sasa wamegundua kwamba Mungu alikuwa sahihi. Mnaona? Mtu hafikirii kwa kichwa chake, akili yake. Yeye ana—yeye ni mtu mwenye utu mara mbili. Tazama, mtu, *hapa* ndani kwanza ni—ni—ni wa kiakili. Lakini wanasema kwamba katika moyo wa mwanadamu, hakiko ndani ya moyo wa mnyama, hakiko kwenye moyo mwingine wowote, lakini moja kwa moja ndani ya moyo wa mwanadamu kuna chumba kidogo katikati ya moyo wa mwanadamu, ambacho hakina hata seli ya damu ndani yake. Lakini ndicho makazi ya nafsi. Kwa hivyo mwanadamu hufikiria kwa moyo wake, sio kwa kichwa chake.

103 Sasa, kama ukiwazia, hiyo ndiyo sababu tuna washiriki wengi vuguvugu wa kanisa siku hizi. Watu wana imani ya kiakili. Watahurumia, waseme, "Loo, Biblia ni ya kweli. Hakika. Naam, bwana." Mnaona? Wana akili ya kusema, "Loo, ninaamini Bwana Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Nimemchukua kama Mwokozi wa kibinafsi": wanavuta sigara, wanakunywa wiski, wanaenda huko nje, wanaenda kwenye madansi, kulala kwenye bandari hizi, na kadhalika karibu na hapa. "Hakika. Kristo ni Mwokozi wangu. Loo, hakika, bila shaka, mimi ni mfuasi wa kanisa." Hiyo ni imani ya kiakili. Watu wengi watakuja kwenye mstari wa maombi na kusema, "Loo, ndugu, nina imani." Hakika, ni imani ya kiakili.

104 Lakini imani hiyo ya kiakili inapoingia kwenye chumba hiki kidogo *hapa*, inakuwa halisi. Mashetani hao wote wa kuzimu hawawezi kuitikisa. Hiyo ni kweli. Inaposhuka *hapa* chini, swali la dhambi limetatuliwa. Amina. Anaposema, "Haya, mimi ndimi Bwana nikuponyaye," hilo linapopitia kwenye imani ya kiakili, lizame kwenye chumba hicho kidogo, hakuna madaktari wa kutosha Chicago watakaokwambia utakufa. Hapana, bwana. La, hasha. Na ikiwa ni wazuri kweli, hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Anaingia moja kwa moja na kuchukua hiyo imani ya kiakili, na kuinena ndani ya moyo wa mwanadamu. Ndipo inapoingia moyoni, inakuwa halisi. Hapo ndipo ambapo Mungu Mwenyewe anapoingia ndani ya moyo wa mwanadamu na kufanya hilo kuwa kweli halisi. Amina. Wakati imani hiyo inapotoka akilini na kuingia katika moyo wa mwanadamu, sasa mnaona ninachomaanisha?

105 Sasa, chini ya damu iliyomwagika, Yeye alisema, "Mchukue ndama huyo, mwenye umri wa miaka mitatu, na hana budi kuwa mwekundu." Nao watampeleka hapa nje. Jambo la kwanza, lazima kamwe awe hajatiwa nira shingoni mwake. Loo, ninapenda hilo kweli. Sasa sikilizeni, huenda hili likachoma na kuunguza na kuchachatika, lakini ni bora kufanya hivyo kwa muda kidogo kuliko kulifanya milele. Angalieni, huyo—huyo ndama alimwakilisha Kristo, naye Kristo hakufungwa nira na chochote (Amina.), bali alikuwa ni Mungu pekee.

106 Sasa, isivyo sawasawa. . .msifungwe nira pamoja na wale wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa, kuenda hapa nje na katika *hii* na *ile*, na kusitasita huku, mkijifunga nira katika karamu hizi na madansi, na kadhalika; kaeni mbali nayo. Jifunge nira pamoja na Kristo. "Jitwikeni nira Yangu; mkajifunze Kwangu."

107 Ndama huyu hangeweza kuwa na nira juu yake. Hana budi kuwa bila nira yoyote juu yake. Na kisha lazima achinjwe mbele ya kuhani mkuu. Ndipo kuhani mkuu, Haruni, alipoona ya kuwa huyo ndama amechinjwa, Eliezeri akatwaa damu kwa kidole chake, akaenda, akaipaka mlangoni mara saba, juu ya mlango wa hema, ushuhuda wa hadharani. Ndipo huyo ndama akachukuliwa na kutiwa motoni na kuchomwa moto: akateketezwa kisha akatolewa nje ya ua (Angalieni, linapendeza. Sina budi kuharakisha.), nje ya ua, hii iliwekwa mahali safi, kwa maana ilikuwa ni maji ya farakano.

108 Katika Waefeso, Paulo alisema hapa, ya kwamba Mungu, kwa kuhubiriwa kwa Neno, yale Maji ya farakano. . .Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia kwa Neno na Neno la Mungu ni Maji ya farakano; kwa maana ni kwa kufanywa upya kwa maji kwa Neno. Kusikia Neno hutenganisha.

109 Sasa, asiyeamini, ama yule mtu mwenye dhambi alikuwa nje. Hii hapa sehemu ndogo ambayo hatutaki kuipita: kwamba

maji ya farakano hayana budi kuwekwa mahali safi. Naye mhubiri anayehubiri Injili anapaswa kuwa mtu safi, mnyofu; sio mwathiriwa wa sigara, si mtawaliwa wa dawa za kulevya, si mlevi, wala mcheza gofu Jumapili alasiri, na kadhalika namna hiyo. Hapana, bwana; hayana budi kuwekwa ndani ya chombo safi kitakatifu kilichotakaswa, yule anayeshikilia siri ya Mungu moyoni mwake.

110 Hayana budi kuwa katika kanisa safi, sio mahali ambapo wanacheza karata kwenye chumba cha chini, bahati nasibu, wana karamu za supu huko nje, na madansi kwa vijana. Mbona, ndugu, kama kamwe ikifikia mahali inaponibidi kufanya hivyo nipate kulishikilia kusanyiko, nitaondoka na kujichukulia mitego kadhaa nihamie Canada, niende kutega nipate riziki. Amina. Ni afadhali kufanya hivyo kuliko kujua kwamba ningepatana juu ya Injili safi isiyoghoshiwa ya Bwana Yesu. Nipe ushirika pamoja Naye. Amina. Lihubiri Neno. Haikubidi uwe na upuuzi huu wote. Dumu na Neno. Nalo Neno huwatenga wenye dhambi na dhambi zao.

111 Ndipo kila mtu nje ya ushirika alipitia kwanza kwenye maji ya farakano katika kusanyiko, naye akanyunyiziwa maji haya. Sasa, ilikuwa ni kitu gani? *Maji* yalinena juu ya dhabihu iliyokufa iliyomtangulia. Yule ndama aliyekufa alikufa badala yake. Nasi tunapohubiri Neno, si juu ya dhehebu lolote, ni juu ya Kristo, yule Dhabihu aliyekufa badala yako, kwa dhambi, badala yake.

112 Uko nje ya ushirika, huwezi kujibiwa maombi, kila kitu ni cheusi karibu nawe: nje ya ushirika. Rudi kwenye Neno sasa. Neno linaanza kukata, linakutenganisha, "Vema, hupaswi kufanya *hivi*, hupaswi kufanya *vile*. *Hili* liko *hapa*. Huna ushirika tena. Umejiondoa kwenye ushirika." Hayo ni maji ya farakano, yanakuambia unachopaswa kufanya.

113 Ndipo muda si muda mwajua, mwaminio, baada ya kufanya jambo hilo, jambo lingine alilofanya, alisonga mbele basi. Anaingia, mwaminio sasa, anasonga mbele. Anapokuja karibu na mlango, anatazama; anaona milia saba ya damu, ambayo ina maana kwamba damu ilimtangulia. Sasa, yeye anakuja chini ya hiyo milia saba ya damu, humo chini ya damu, halafu ana ushirika (Mnaona hilo?), ushirika pamoja na Mungu, hakuna ushirika mahali pengine popote. Na kitu hicho chote katika lile hema, katika kuhesabiwa haki chini ya ua, utakaso madhabahuni, Roho Mtakatifu nyuma ya pazia, pale alipoingia na kuishusha: yote ni picha ya Kristo.

Haijalishi waliunda madhehebu jinsi gani; Kora aliunda shirika, akasema, "Kuna watu wengi zaidi watakatifu kuliko Musa, kwa hiyo tutatoka tu . . . "

114 Mungu alisema, "Jitenge naye, sasa hivi, maana amevunja mpango wa Mungu." Mnaona? Ushirika ulikuwa mahali pamoja

tu; hapo ni chini ya damu iliyomwagika.

115 Sasa sikilizeni, enyi Wakristo, kwa makini. Tazama. Hakuna ushirika nje ya Mwili wa Yesu Kristo, huwezi kuwa na ushirika pamoja na Mungu. Si ajabu watu hawaamini katika uponyaji wa Kiungu. Si ajabu hawawezi kuamini katika uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu. Si ajabu hawawezi kuamini katika mambo haya yanayousafisha moyo wa mtu. Huna budi kuingia kwanza kwenye ushirika kabla ya kuelewa mambo haya. Ingia ndani, lisikie Neno; linakutenganisha, linakuosha. Kisha uingie chini ya Damu ndani ya Mwili wa Kristo.

Ambapo lile hema lilikuwa mfano kamili wa Kristo: "Livunjeni jengo hili, nitalijenga katika siku tatu tena." Mnaona? Alikuwa.

116 Na halafu kwa Roho mmoja, sote tunaongozwa na Roho Mtakatifu kuingia katika Mwili wa Kristo, na kisha tunaingia chini ya Damu. Maswali yote ya dhambi yalitatuliwa kwa nje, kwa kuhubiriwa kwa Neno, kwa dhabihu ya—ya Mwana-Kondoo madhabahuni. Na sasa tuko katika ushirika pamoja na Kristo na tunaweza kuingia na kuwasiliana na hao wengine.

117 Wale walio ndani ya hili jengo katika Kristo, tunaingia. Wakati mmoja ulimwita mtakatifu anayejifingirisha. Wakati mmoja ulisema, "Ana kichaa, amerukwa na akili." Lakini wakati wowote unapokuja chini ya Damu iliyomwagika na kufanya ushirika, unamwendea mwanamume huyo ambaye hapo awali ulidhani alipiga kelele sana, mwanamke huyo uliye-. . .uliyemsikia akipaza sauti usiku ule, yule jirani uliyemsengenya, ama aliyekuja kukuambia juu ya uponyaji wa Kiungu, utatamani kuweka mkono wako katika mkono wa huyo mwanamume ama mwanamke, na kuwa na Neno la ushirika. Kwa nini? Umekuja chini ya Damu.

118 "Pasipo kumwaga Damu, hakuna ondoleo la dhambi." Haidhuru wewe ni mwema kiasi gani, unashiriki kanisa gani, unakariri kanuni gani ya imani, maombi gani unayofanya, isipokuwa uje chini ya Damu, bado uko nje ya ushirika pamoja na Mungu.

119 Je, lisingekuwa jambo la ajabu sasa kama kundi zima letu papa hapa, kama watu mia sita, au, mia tano au mia sita, wowote walio katika kusanyiko hili, watu hawa wote pamoja alasiri ya leo, sisi kwa nia moja tungeweza kuja moja kwa moja chini ya Damu, kama tu vile tulivyo chini ya paa hili hapa, chini ya Damu ya Bwana Yesu Kristo, unafikiri nini kingetukia sasa hivi? Unafikiri nini kingetukia? Mbona, kusingekuwako na mtu mnyonge kati yetu katika dakika tano zijazo. Loo, jamani. Mwenye dhambi anayeketi karibu nawe angehukumiwa sana, asingeweza hata kusimama wima tena, Roho Mtakatifu akizunguka, maji ya farakano yakimiminwa, Injili, akimhubiri Bwana Yesu Kristo, katika Dhabihu Yake kuu. Na nguvu za

uponyaji zikishuka kupitia Kalvari, mbona, tungekuwa tu na wakati wa ajabu, sivyo? Hilo si lingekuwa ni jambo zuri sana, kama sote tungeweza kuingia katika ushirika? Ni wangapi wangependa kuwa katika ushirika huo? Inua mkono wako.

120 Sasa, sikilizeni, marafiki. Nimezungumza mambo magumu alasiri ya leo kuhusu madhehebu. Sasa, sio kwamba ninayapinga madhehebu. Mungu anajua hiyo ni kweli. Sijali kuhusu madhehebu. Lakini jambo ni kwamba, unapofikiri kwamba dhehebu hilo litakufanyia jambo fulani, sivyo. Damu ya Yesu Kristo ndiyo Kitu pekee kingeweza kukufanyia jambo. Hiyo ni kweli. Na ndipo wakati Damu hiyo inapoingia moyoni mwako, mawazo yako yote ya kiakili ni tofauti, kwa sababu unawazia kutoka *hapa* basi. Unaona?

121 *Hapa* ndipo Kristo anapokuja, moyoni. Na mawazo yako ni mazuri. Sio, "Vema, Bi Jones alisema kwamba angeweza kwenda kwenye madansi, halikumsumbua." Unaona? Unawazia kuhusu Bi Jones. Lakini inapokuwa moyoni, unawaza juu ya Bwana Yesu, kile ambacho angefanya. Unaona, mawazo yako yote yamerudi *hapa* tena. Na hicho ndicho tunachohitaji siku hizi, ni ushirika huu wa ajabu wa Bwana Yesu Kristo, na Mungu akirudi katikati yetu akizungumza nasi.

122 Sasa angalia, sasa, kama nyota hizo ndizo. . . Nilikuwa nikiweka muda hivi majuzi, kwenye chumba cha uchunguzi. . . Kabla tu sijafunga nataka niwapeni wazo. Ikiwa nyota hizo, walisema ingenichukua. . . nuru, ikisafiri, nasahau ni maelfu mangapi ya miaka, kwa mwendo, kusafiri kwa mwendo wa nuru, nuru ikisafiri mbio hivyo, kuja hapa duniani. Maelfu mara maelfu mara maelfu mara maelfu ya miaka, kwa mwendo wa nuru, kufika hapa duniani kutoka kwa mojawapo ya nyota hizo. Na tunaweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga ya nuru, na kupita hapo ni nyota tupu kama ilivyo hapa. Je, ingemchukua Malaika muda gani kutoka huko, kufika hapa?

123 Sasa, ukizungumza juu ya Mbingu, au tunapokufa, kwamba tunaenda mahali fulani ambapo hata huwezi kuona huko juu, hivi huoni kwamba Munguameficha utukufu kutoka kwa jicho la kawaida?

124 Tumeketi hapa katika mahali pa Mbinguni. Sasa Roho Mtakatifu yuko hapa. Sasa Kristo yuko hapa. Nao mwili tunaopokea tunapotoka hapa, tunaingia katika kiwango kingine, mahali penye baraka pamoja na Bwana Yesu, na katika kurudi kwa Kristo katika mwili Wake wa kawaida akirudi duniani, roho hizi zitarudi na kuchukua mwili mpya kabisa tena nasi tuishi milele. Amina. Loo, jamani. Kama watu wangeweza kupata wazo sasa hivi, la Malaika wakitembea huku na huko kwenye marefu hayo ya kanisa, la Kristo, Mwana wa Mungu, akizungukazunguka humu jengoni (Loo, jamani.), ni tofauti jinsi gani. Mko Mbele Zake.

125 Ndipo wakati roho yako inapotiwa nguvu sana kwenye ulimwengu huo wa nje, na kama tu vile su—sumaku, au, fuwele kwenye redio na wakati kifaa hicho mle ndani kinapochajiwa sana au kutiwa sumaku kwenye maneno hayo, kinanyooka, mpaka kinaipiga na kuyafanya halisi. . .Redio, ikipitia hapa, yale maneno, hatuwezi kuyasikia kwa masikio yetu, yapo. . .hatuwezi kuyashika. Lakini fuwele hiyo kwenye redio huyashika, televisheni vivyo hivyo. Yanakuwa halisi.

126 Ndipo imani yetu ya kiakili inaposhuka moyoni, basi inachajiwa sana na ulimwengu usioonekana, hata kila Neno la Mungu linakuwa ukweli halisi. Mnaona ninachomaanisha?

127 Mungu anaposema jambo, linarudisha mwangwi dhidi yake, kama tu linavyofanya kwenye fuwele hiyo katika redio, na kulifanya kamilifu. Mungu alisema, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Hilo latosha. Amina. Hilo linalifanya halisi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu." Hilo linalifanya halisi, Yeye yuko hapa sasa. Sasa, hivyo ndivyo ilivyo mahali ninapopelekwa katika uponyaji wa Kiungu.

128 Wakati yule Malaika wa Bwana alipotokea usiku ule, kasema, "Nitakuwa pamoja nawe; usiogope." Yale angefanya; alisema angeonyesha ishara na maajabu miongoni mwa watu.

Nilimhoji. Nikasema, "Mimi. . .Hawataamini hilo."

129 Akasema, "Itakuwa, ya kwamba utajua hata siri zenyewe za mioyo yao, uwaambie mambo haya." Nami nilihoji hilo. Akalirejesha kwa Kristo. Akasema, "Nitakuwa pamoja nawe." Ndipo ninapoenda jukwaani, watu wagonjwa, ama kitu kingine kama hicho juu ya mambo hayo, linakuwa ni jambo la kweli. Ninaliamini.

130 Laiti ningelikuwa na imani sasa hivi kuamini kwamba kila mgonjwa katika jengo hili angeponywa, kama vile tu nilivyo na imani ya kujua ya kwamba Yeye amesimama papa hapa. Laiti ningalikuwa na imani ya aina hiyo, laiti kila mmoja wenu angekuwa nayo. Lakini mawazo yetu na ushirika wetu ukitoka katika milki za vitu tunavyoona kuingia kwenye vitu tusivyoviona, basi unakuwa hakika tu kama vile vitu tunavyoona, au hakika zaidi.

Bwana na awabariki tunapoinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja.

131 Baba wa Mbinguni, loo, kwa ajili ya ushirika wa Mwili wa Kristo, kwenye Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno naye Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu; naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Loo, jinsi tunavyompenda; jinsi tunavyothamini Uwepo Wake hapa sasa, Mwana mkuu wa Mungu, Yeye aliyefufuka, ambaye Maneno Yake hayawezi kushindwa kamwe, imeandikwa hapa katika

Biblia, kwamba, "popote walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Na Yeye yuko hapa.

132 Mungu, jalia kila asiyeamini ambaye hajafanywa upya, hajapitia kwa Damu, amekuwa tu akienda kanisani, angali ana hasira, angali ana tabia za ulimwengu wanayoshikilia, imani ya kiakili, lakini kamwe hawajaoshwa na kutakaswa wapate kuwa na ushirika mkamilifu, Mungu, jalia alasiri ya leo kwamba sasa hivi mahali hapa, kwamba kila moyo utaoshwa, na kusafishwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Wataingia katika ushirika hata ibada ya uponyaji ya usiku wa leo itasababisha mkutano mkuu zaidi ambao umewahi kufanyika katika kusanyiko hili. Tujalie, Bwana. Je, utafanya hivyo? Kwa utukufu wa Mungu, tunaomba.

133 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nashangaa, huku kila mtu akiomba tu, mkipenda. Najua muda unaenda, lakini tazameni, marafiki, muda unaenda kwa njia mbili: Siku imeenda sana, Jumapili alasiri siku hii, siku ya kwanza ya Mei; nao wakati umeenda sana, pia. Muda umeenda kuliko vile tunavyofikiri. Kuja kwa Bwana kumekaribia; mioyo ya watu; mnaona ustaarabu huu mkuu ukianguka, ukizama sasa hivi. Angalieni tu Marekani hii. Ni fedheha jinsi gani. Angalia yale Yesu aliyosema, "Katika siku za mwisho kama ilivyokuwa kwa Nuhu, watakuwa wakiolewa na kadhalika."

134 Angalia mahakama za talaka Marekani ni kubwa kuliko mataifa yote yakiwekwa pamoja. Angalia utovu wa uadilifu; angalia upotovu wa vilabu vya upotovu wa kijinsia huko Pwani ya Magharibi, na pande zote. Maelfu mara maelfu wakienda kila mwaka. Kinyaa, uchafu, uovu, wakichukua matumizi ya asili ya mwili na kuyapotosha yakawa kitu fulani, watu wenye akili potovu. Wanaume hutoka na kufanya yasiyofaa jinsi wanavyofanya, wanawake wakivaa maskini nguo hizi fupi sana huko nje, hawadhani wamekosea. Bila shaka, nia zao zimepotoshwa; ibilisi amewashika; hawana habari. Sasa, ni siku ya jinsi gani?

135 Je, uko chini ya Damu, mwaminio? Kama sivyo. . . wakati, acha mimi pamoja na Bwana Yesu peke yetu tuangalie hili. Kama kuna mtu hapa, mwaminifu moyoni mwako, na anayejua, na kwa kuhubiriwa kwa Neno, umeamini hili, kwamba umekosea, kwamba kitu Fulani moyoni mwako kinakwambia kwamba umekosea, endapo ungali na mambo haya, na unatamani mambo hayo. . . Huninii, sio lazima uyafanye, ikubidi kuyafanya, ni kuwa tu na shauku yake. Unaona? "Amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini pamoja naye moyoni mwake."

136 Si yule anayechukua bunduki na kumpiga risasi ndugu yake, lakini "anayemkasirikia bila sababu." Ikiwa unajua umekosea, unaweza kuinua mkono wako? Unasema, "Ndugu Branham,

niombee sasa. Ninaomba ya kwamba Mungu atanileta chini ya Damu, na kunipa tukio la mtindo wa kale na moyo wangu uwe safi mbele za Mungu." Kama mtu huyo yuko hapa ndani, waweza kuinua mkono wako, sasa hivi, kabla hatujaomba? Na kusema, kwa kuinua tu mkono wako, si kwangu, bali kwa Mungu, useme, "Mungu, unirehemu sasa; nataka moyo safi kabisa mbele Zako."

137 Je, kuna mtu mahali popote kwenye roshani au popote? Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu akubariki, dada yangu. Hilo ni jema. Sasa, Mungu akubariki, ndugu yangu. Hilo ni sawa. Uwe mwaminifu kwa Mungu.

138 Sasa, sio—sio mimi. Hamniinulii mimi mikono yenu, mnamwinulia Mungu. Mungu akubariki, mama; Nakuona huko nyuma. Mtu mwingine ambaye...? Mungu akubariki, mama; na wewe, bwana; na wewe, bwana. Mungu akubariki; na wewe, bwana. Hiyo ndiyo njia ya kuwa mwaminifu. Hiyo ndiyo njia ya kuwa wanaume na wanawake; tuko mbele za Mungu.

139 Mungu akubariki, mama. Unataka mambo hayo yaondolewe maishani mwako. Hakika, Mungu atafanya hivyo. Jambo pekee unalopaswa kufanya, ni, kumwacha tu afanye hivyo sasa. Je, kuna mwingine kabla ya maombi?

Huku tumeinamisha vichwa vyetu.

140 Mungu mpendwa, Ee Baba, roho hizo za wanadamu, tunatambua Bwana ya kwamba hapa katika jengo yupo Yeye Yule atakayetuhukumu katika Siku hiyo. Hata shomoro hawezi kuanguka barabarani pasipo Baba kujua. Ni zaidi sana vipi unawajua watu hawa wanaoinua mikono yao kwa uaminifu, wanaoketi hapa katika saa hizi zilizoenda sana za alasiri, wakilisikiliza Neno. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utausafisha kila moyo sasa hivi kwa Damu ya Bwana Yesu. Jalia kila tabia, kila dhambi ya ukandamizaji, au shida yoyote waliyo nayo watu hawa wapendwa, Mungu, ninaomba ya kwamba utaiondoa kwao sasa hivi. Lijalie. Jalia wawe Wakristo wanyenyekevu, watamu, wanaochukia uovu na kupenda haki. Tujalie, Baba. Ewe Mwokozi uliyebarikiwa uwaongoze.

141 Sasa, Baba, jalia kila mtu hapa ndani apokee imani kuu sasa hivi. Tunatazamia ibada ya usiku wa leo, Bwana, kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa. Loo, utaruhusu mara moja tu tena, Bwana, mara moja tena litukie? Kwenye mkesha wa ndugu yetu kwenda katika nchi za ng'ambo, apate kwenda na ono jipya moyoni mwake auone Ufalme wa Mungu ukiletwa mbele ya watoto wa wanadamu.

142 Jalia hii iwe ibada nzuri sana usiku wa leo; jalia kila mgonjwa aingiaye katika mlango wa Kristo aponywe kikamilifu. Je, utatujalia, Bwana? Waponye walio wahitaji; wazima mwilini; kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

143 Imekuwa siku chache sana, nimekuwa nyumbani, nilikuwa na shida nyingi na kadhalika, mnajua jinsi kulivyo nyumbani. Nilikuwa macho usiku wa kuamkia jana hadi mapambazuko, nikaingia, nilikuwa nje siku nzima jana. Jana usiku, usingizi kidogo sana, ndipo nikaamka asubuhi ya leo nikaja huku. Ni ngumu kwa namna fulani. Nimewaweka muda mrefu. Samahani niliwaweka muda wote huo. Natumaini ninyi. . . ni Roho Mtakatifu. . .Nimeona. Nataka kusema hivi, kama. . . Afadhali nikupe tumba dogo la waridi sasa kuliko shada zima ukiisha kuondoka. Unaona?

144 Sijawahi. . .Nimekuwa na makusanyiko mazuri kote ulimwenguni. Lakini sijawahi kuwa na ku—kusanyiko makini zaidi kuliko nililo nalo hapa katika kanisa hili dogo hapa Chicago, ninyi watu wa hapa. Ninaona alasiri ya leo, nilikuwa nalo moyoni mwangu, nilipokuja jukwaani, kuzungumza juu ya jambo lingine. Kweli Roho Mtakatifu alikuwa akiniambia ku. . . juu—juu ya Sanduku la Agano, kile ambacho ningezungumzia. Ndipo nilipokuja jukwaani hapa juu, niliwaza, "*Ushirika* ungekuwa ni jambo zuri kuzungumzia."

145 Nimefanya jambo ambalo, ni, nikavuka mwenyewe mahali ambapo Roho Mtakatifu alikuwa ameniambia nisivuke, lakini nilijaribu kupambana kote. Hebu niwaambieni jambo fulani, na yale niliyosema kuhusu Ndugu Joseph dakika chache zilizopita, wakati niwapo makosani, niwe sahihi ama nisiwe sahihi. Vivyo hivyo nanyi, hapajakuwa na mtu aliyeamka na kuondoka kwenye jengo hili alasiri ya leo. Wakati wote wangeweza kuwa wameketi hapa, wakati wote wakijua ya kwamba ibada ya uponyaji inakuja, na wengi bado hawajaenda nyumbani na kula chakula cha jioni. Mumeketi papa hapa pamoja nami. Nawatakia heri. Nawapenda. Nitawapeleka mbele za Mungu. Nanyi mumelishikilia hapa wakati mumeniona hata nikipiga vita. Mnaona, hilo ndilo ninalomaanisha: ninapokosea wakati mwingine (Mnaona?) ninapokuwa makosani.

146 Sasa, ninaomba ya kwamba Mungu atawapa kila kitu mnachohitaji, kila shauku ya moyo wenu. Na naomba. . .Ni wangapi hapa ndani wanaotaka kuponywa usiku wa leo? inua mkono wako; kila mtu tu humu jengoni. Mungu awabariki. Loo, jamani, neema Yake na iwe pamoja nanyi. Sasa, ikiwa itabidi uende nyumbani, naomba uende ukapumzike kidogo. Rudi, baada ya kitambo kidogo, uichukue kadi ya maombi, uje usiku wa leo ukaombewe. Ninaamini tu tutakuwa na mkutano mzuri sana, sivyo? Amina, amina. Mungu awabariki. Ninairudisha ibada sasa kwa Ndugu Joseph. Nitawaona baada ya saa chache.

55-0501A Ushirika
Philadelphia Church
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org